Toleo 5

# Ukweli wa Injili

MAFUNDISHO YA BIBLIA NA HIMIZO KWA KAZI YA KIMISHENI ULIMWENGUNI KOTE

## TAZAMA, NAJA UPESI

"Maana hatukufuata hadithi zilizo-tungwa kwa werevu, tulipowajulisha ninyi nguvu zake Bwana wetu Yesu Kristo na kuja kwake; bali tulikuwa tumeuona wenyewe ukuu wake...Nasi tuna lile neno la unabii lililo imara zaidi, ambalo, mkiliangalia, kama taa ing'aayo mahali penye giza, mwafanya vyema, mpaka kutakapopambazuka, na nyota ya asubuhi kuzuka mioyoni mwenu" (2 Petro 1:16, 19).

Imani na maisha ya Mkristo hainawiri juu ya hadithi za kubuni au za simulizi ambazo hazina ukweli ndani yake, bali yamesimama juu ya kutimia kamili kwa zaidi ya unabii 2,000 ambao ulitabiriwa kwa kipindi cha miaka mia kadhaa. Unabii huo wa kale ulitabiri kwa njia sawasawa kabisa kuhusiana na kuzaliwa, maisha, kifo, na kufufuka kwa Masiya Yesu Kristo. Sayansi ya uwezekano wa mambo (kufanyika) inabatilisha dhana ya kwamba mambo hufanyika kwa kutotarajiwa. Mambo yaliyotabiriwa katika Biblia yalifanyika kulingana na vile ilivyotabiriwa. Biblia ni kitabu cha kipekee kati ya vitabu vingine vyote duniani ambavyo vishawahi kuandikwa; Biblia ni ya kweli, ya kutegemewa, yenye nguvu, na ambayo inayosema yatafanyika hufanyika.

Lakini kungali kunazo nabii kadhaa zinazohusiana na mwisho wa ulimwengu ambazo bado



*"Usikawie, kutayarisha roho yako kwa ajili ya maisha ya milele."*

hazijatimizwa. Kwa sababu tunajua kwamba Biblia ni kitabu ambacho kinaweza kutegemewa ni nani anaweza kupuuza mambo yatakayojiri? Wakati mgumu sana unajiri ulimwenguni. Unabii wa mwisho sasa unatimizwa. Ulimwengu unazidi kuzorota katika uovu na ishara za wakati wetu zinaonyesha kwamba ulimwengu huu hautaendelea kudumu muda mwingi zaidi. Hizi ni siku za mwisho katika siku za mwisho. Yesu anarudi mara ya pili ili kuwafikisha wanadamu kwenye kiti cha hukumu ambamo kila mtu atahukumiwa kulingana na kazi zake (Mathayo 16:27). Kama ambavyo unabii ulitimizwa kwa kuja kwa Yesu mara ya kwanza ulimwenguni, ndivyo ambavyo unabii unaosema kuhusu kuja kwake mara ya pili utatimizwa.

Watu wanaishi kama kwamba maisha haya ya sasa yatadumu milele. Wanadamu wanampatia Mungu mgongo na kuishi dhambini bila hofu au kuwaza kuhusu maisha yao ya milele. Yesu anakuja kama "kama mwivi; katika siku (usiku)" (2 Petro 3:10). Ulimwengu utaisha katika wakati ambapo hakuna mtu anatarajia, na hapo ndipo tutasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu ili kupokea adhabu au

*(Inaendelea kutoka ukurasa 2)*


Tahariri 3

Kujifunza Biblia: Mwisho wa Nyakati 4

Mwisho wa Nyakati 5

Swali na Jibu 7

Je, Wajua? Neno Linalofaa kwa Msimu Huu 8

# Mambo Ambayo **BIBLIA** Inafundisha Kuhusu...

**Neno la Mungu**
2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35
**Uhusiano wa Upendo**
Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, 1 Yoh. 4:7-21
**Toba**
Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10
**Uzao Mpya**
Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4, Efe. 2:1, 5-6
**Uhuru Kutokana na Dhambi**
1 Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11
**Ujazo wa Roho Mtakatifu**
Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8
**Utakatifu**
Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, 1 Pet. 1:15-16, Tit. 2:11-12, Rum. 6:22
**Ufalme wa Mungu**
Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36
**Kanisa**
Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, 1 Kor. 12:12-13, Kol. 1:18
**Umoja**
Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4
**Kanuni za Kanisa**
Mt. 28:19-20, 26:26-30, 1 Kor. 11:23-27, Yn. 13:14-17
**Uponyaji wa Kiungu**
Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16
**Utakatifu wa Ndoa**
Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3, 1 Kor. 7:10-11
**Urembo wa Nje**
1 Tim. 2:9-10, 1 Kor. 11:14-15, Kum. 22:5
**Mwisho wa Nyakati**
2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10, Mt. 25:31-46
**Kupenda Amani**
Lk. 6:27-29, 18:20
**Ibada**
Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17
**Wajibu Mkuu**
Mk. 16:15

*(Endelea kutoka ukurasa 1)*

thawabu ya milele (1 Wakorintho 15:51-53). Kwa sababu ya subira zake nyingi Mungu amechelewesha hukumu zake kwa "maana hapendi mtu ye yote apotee, bali wote wafikilie toba"
(2 Petro 3:9).

Baada ya kufufuka kwake Yesu alipaa kwenda mbinguni na ndipo malaika wa Bwana aliwazungumzia wanafunzi wake na kuwaambia: "Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja jinsi iyo hiyo mlivyomwona akienda zake mbinguni" (Matendo 1:11). Yesu anarudi tena. Akija hakutakuwa na wakati wa kutubu, wa kuomba, na hata wa mtu kubadilisha maisha yake. Kila mtu atasimama mbele zake Mungu kama alivyo.

"Tazama, naja upesi, na ujira wangu u pamoja nami, kumlipa kila mtu kama kazi yake ilivyo" (Ufunuo 22:12). Je, wewe wasikia maneno yake Kristo? "TAZAMA, NAJA UPESI." Hakuna muda mwingi uliobaki katika ulimwengu huu wa dhambi. Utaratibu wa hukumu zake Mungu hapo mbeleni kati ya wanadamu unaonyesha kwamba ulimwengu huu umezidisha wakati wake. Wakati ni mfupi. Hakuna uhakika wa kesho kuja. Je, wewe u tayari kukutana na Mungu?

Punde si punde Yesu arudi tena. Basi wewe usikawie kutayarisha roho yako kwa ajili ya maisha ya milele. "Wakati uliokubalika ndio sasa; tazama, siku ya wokovu ndiyo sasa" (2 Wakorintho 6:2). Kama wewe hujaokoka achana na dhambi zako wakati kungali na wakati na nafasi ya kuokoka kupitia kwa damu yake Yesu Kristo. —mws

## UKWELI WA INJILI

Gazeti la '*Ukweli wa Injili*' huchapishwa kwa jina la Bwana kwa matumizi ya watu wa mataifa yote kwa kusudi la kuimarisha na kuwahimiza watu wote katika ukweli wa neno la Mungu. Gazeti hili hufundisha na kueneza ukweli wa Biblia ambao umethibitishwa tangu nyakati za Yesu Kristo na mitume.

Neno la Mungu ndio mwongozo halisi na wa kipekee wa imani. Linafundisha wokovu na ukombozi kutokana na dhambi unaoletwa na utakaso wa Yesu Kristo; ambao hufuatiwa na ujazo wa Roho Mtakatifu anayemwongoza mhudumu, kumwonyesha njia, na kumpatia nguvu; pia unamletea mtu utakatifu halisi katika kila fani ya maisha yake; na pia kuleta umoja na utangamano wa watu wa Mungu. Huduma inayokubalika na Mungu inatokana na mtu kuwa na uhusiano wa kibinafsi na wa upendo ambao msingi wake ni ukweli.

Waandishi: Michael na René Smith

## UAGIJAJI

*Ukweli wa Injili* ni gazeti la kieletroniki linalochapishwa kila robo ya mwaka kwa jinsi Mungu anavyotuongoza. Tutembelee katika tovuti yetu ya www.thegospeltruth.org ili uagize jalida hili kupitia kwa orodha yetu ya anwani pepe na upokee toleo lako la wakati huu. Hebu jisikie huru kututumia orodha ya majina na anwani pepe za watu wengine ambao wangependa kupokea toleo hili kutoka kwa mwandishi wa jalida la Ukweli wa Injili.

## WASILIANA NASI

Gazeti a *Ukweli wa injili* linachapishwa katika mataifa mbalimbali ili kusambazwa katika maeneo hayo. Kazi hii na zingine za kimishenari ambazo sisi hufanya huwezekana kupitia kwa matoleo ya kujitolea yanayotolewa kwa jina la Kanisa la Mungu.

The Gospel Truth, PO Box 2042, Nixa, MO 65714 USA
editor@thegospeltruth.org

# Tahariri



*"Naja upesi. Shika sana ulicho nacho, asije mtu akaitwaa taji yako"* (Ufuno 3:11).

Kwa miezi kadhaa nimekuwa na mzigo mkubwa rohoni mwangu unaniambia kwamba wakati wetu hapa duniani unakwisha haraka. Mimi siamini kwamba Bwana atacheleweshа kurudi kwake kwa muda zaidi. Ujumbe wa kurudi kwa Bwana unabisha sana moyoni mwangu.

Ninakumbuka kuhusu nabii Yesu mwana wa Anania ambaye alitembea katika barabara za mji wa Yerusalemu huku akipaza sauti kuhusiana na maangamizi ya mji huo kabla ya Mungu kuuangamiza: "Ole kwako ewe Yerusalemu." Watu walijaribu kusema yeye ni mwendazimu na wakajaribu kumnyamazisha. Mji wenyewe ulionekana kuwa na amani na uliendelea kutajirika, lakini yeye aliendelea kufanya kilio: "Ole wenu, ole wenu—sauti inalia kutoka mashariki, sauti kutoka magharibu, sauti kutoka kwa upepo wa pande zote nne, sauti dhidi ya mji wa Yerusalemu..." Yeye alitabiri kwa muda wa miaka saba na miezi mitano. Halafu unabii ukatimizwa na maangamizi yakaufikia mji wa Yerusalemu.

Watu wanaweza kudhihaki na kuchoshwa na ujumbe huu, lakini mimi niko tayari kuwa Anania. Wakati ni mfupi. Bwana arudi haraka. Wewe endelea kushikilia unayoamini na uwe mtu wa kweli. Ishi kila siku kama kwamba ni siku yako ya mwisho, kwa sababu punde si punde itakuwa hivyo. Ulimwengu unazidi kuzorota na athari za Shetani zaendelea kuwa nyingi kati yetu sote. Lakini kungali na nguvu za kumwezesha mtu kuishi maisha matakatifu na masafi kupitia kwa Yesu Kristo, lakini pia tunahitaji kuishi karibu na masalaba.

Toleo hili la *Ukweli wa Injili* linashughulikia swala la Kristo kuja mara ya pili na kuhusu mwisho wa nyakati. Kuna hali kubwa ya kutokuelewa na mafundisho ya uongo kuhusiana na swala hili. Tunahitaji kutazama mambo kulingana na Neno la Mungu na kulihubiri kwa ukweli. Silaha bora kabisa ya kukabiliana na upotovu wa ukweli ni ukweli wenyewe. Lakini hili ni somo kubwa na uhaba wa nafasi kwenye jalida hili hauniruhusu kuchunguza maandiko yote yanayohusiana na swala hili. Walakini hakukuwa na nafasi ya kuandika kuhusu baadhi ya unabii kwenye kitabu cha Ufunuo ambao umeleta hali kubwa ya kuchanganyikiwa katika mafundisho ya "Siku za Mwisho." Katika usomaji wa Neno la Mungu ni jambo muhimu kuchukua mambo yaliyo rahisi na wazi na kuyatumia kama mwongozo wa kuelewa unabii na lugha ya kimfano ambayo ni ngumu zaidi kwenye kitabu cha Ufunuo.

Kuna maelezo mengine ambayo pengine Mungu alitufícha kwenye Biblia, lakini ametupatia miongoza inayotosha ya kutufikisha mbinguni. Mamilioni ya watu wamehadaliwa na kuamini tumaini la uongo la kuweko na ufalme wa baadaye. Jambo hili nalo huwafanya kutomtafuta Bwana kwa moyo wao wote maishani.

Tunakuomba uendelee kuomba ili sisi tupate uongozi wa Bwana na baraka zake katika kazi tunayofanya kwenye jalida la *Ukweli wa Injili na Umisheni wa Kiafrika na Zaidi*. Sisi kila siku tunategemea Roho wa Bwana kukutana na mahitaji yetu na kutuongoza kazini mwake.

Muda ni mfupi. Muda si muda Yesu yuaja.

Michael W. Smith

Julai 2013

mengi kwa MTANDAO

*Tutembelee kwa*

*www.thegospeltruth.org*

*ili uagize na kusoma*

*jarida letu.*



## KUACHWA NYUMA?

*Kama moto wa pori mafundisho kuhusiana na kunyakuliwa tena yamesambaa kote ulimwenguni.* Neno "kunyakuliwa" lina maana ya "kushikwa huko juu" au "kubebwa kupelekwa mbali." Makundi mengi ya Kikristo hufundisha kwamba watakatifu watachukuliwa huko juu na Bwana, na kupelekwa mbinguni, wakati ambapo wasio watakatifu "wataachwa nyuma" hapa duniani ili kupata wakati wa mateso.

Maandiko ambayo hutumiwa kufundisha hivyo ni 1 Wathesalonike 4:16-17 ambayo husema: "Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni . . . nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza. Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani..."

Hapa mtume Paulo alikuwa akisema na watakatifu kwa njia ya moja kwa moja kwa maana aliwaambia "farijianeni kwa maneno hayo." Hakuwa akinena kuhusu hatma ya wale ambao sio wacha Mungu. Yesu alisema "wote waliomo makaburini wataisikia sauti yake. Nao watatoka…" (Yohana 5:28-29).

Kutakuwa na ufufuno mmoja wa watu wote na hukumu moja ya watu wote. Hakuna mtu atakayeachwa nyuma, kwani sisi wote tutasimama mbele ya kiti cha hukumu chake Mungu.

# MWONGOZO WA KUJIFUNZA BIBLIA

## SOMO: MAFUNDISHO YA BIBLIA KUHUSU MWISHO WA NYAKATI

**Somo la Biblia:**
Yakobo 5:8 *Nanyi vumilieni, mthibitishe mioyo yenu, kwa maana kuja kwake Bwana kunakaribia*.

**Muhstasari:** Yesu Kristo atarudi mara ya pili duniani wakati ambapo watu wote watafufuka na kupelekwa mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu. Ulimwengu huu utaangamizwa na watakatifu wataishi milele mbinguni, na wale wasio watakatifu wataishi jehanamu.

**I. Kuja kwa Pili kwa Kristo**

A. Yohana 14:28 Yesu aja tena.
B. Matendo 1:9-11 Kwa njia ya waziwazi.
C. 1 Wathesalonike 5:2 Kama mwizi.
D. Mariko 13:32 Wakati haujulikani.
E. Luka 12:40 Bila kutarajiwa.
F. Ufunuo 1:7 Kila jicho litamwona.
G. 1 Wathesalonike 4:16 Kwa mwaliko.

**II. Ufufuo Mmoja wa Wote**

A. Yohana 5:28-29 Wote walio makaburini.
B. Matendo 24:15 Ya wenye haki na wasio na haki.
C. 1 Wathesalonike 4:16-18 Watakatifu kwanza.
D. 1 Wakorintho 15:51-53 Tutafufuliwa kwa mwili usio na uharibifu.

**III. Maangamizi ya Dunia**

A. 2 Petero 3:7-12 Ulimwengu utachomwa wote.
B. Mathayo 24:35 Utapita.
C. Waebrania 1:10-11 Utaangamia.

**IV. Hukumu ya Watu Wote**

A. 2 Wakorintho 5:10 Watu wote watahukumiwa.
B. Yohana 12:48 Kuhukumiwa siku ya mwisho.
C. Matendo 17:31 Ulimwengu kuhukumiwa na Kristo.
D. 2 Timotheo 4:1 Walio hai na wafu wahukumiwa.
E. Warumi 14:10-12 Kuwajibika kwa kila mtu.
F. Mhubiri 12:14 Siri za watu zahukumiwa.

**V. Maonyesho Kuhusiana na Hukumu (Hukumu, Thawabu na Adhabu)**

A. Mathayo 25:31-46
B. Ufunuo 20:11-15

**VI. Kiwango cha Adhabu**

A. Warumi 2:6 Kulingana na matendo ya mtu.
B. Luka 12:47-48 Kiasi.
C. Tazama pia: 2 Petro 2:21; Waebrania 10:29

**VII. Adhabu ya Milele – Jehanamu**

A. Tazama *Maonyesho Kuhusiana na Hukumu.*
B. Zaburi 9:7 Jehanamu.
C. 2 Petro 2:9 Adhabu.
D. 2 Wathesalonike 1:9 Ya milele.
E. Mathayo 24:50-51 Kilio.
F. Ufunuo 21:8 Moto na kiberiti.
G. Luka 16:23-26 Mateso ya Jehanamu.

**VIII. Thawabu ya Milele – Mbinguni**

A. Tazama *Maonyesho ya Hukumu.*
B. 1 Petro 1:4-5 Urithi huko mbinguni.
C. 2 Wakorintho 5:1 Yenye kuundwa bila matumizi ya mikono ya wanadamu.
D. Waebrania 11:16 Nchi ya mbinguni.
E. Ufunuo 7:15-17 Bila njaa au majonzi.
F. Ufunuo 21 na **22** Maelezo.

**Tamati**
Ufunuo 22:20 Yeye mwenye kuyashuhudia haya asema, Naam; naja upesi. Amina; na uje, Bwana Yesu

# MWISHO WA NYAKATI

*Nakala ya Kuandamana na Mafunzo ya Biblia*

### Maandiko nido mwogozo wetu

Kuja kwa pili kwa Kristo na matukio yatakayofuata ni mambo muhimu sana. Kuna maandiko mengi na unabii mwingi kuhusiana na nyakati za mwisho. D.S. Warner alisema kwamba, “Dhana ya mtu au kutaka kubahatisha si mambo yenye maana yoyote kuhusiana naa mambo yatakayokuja.” Ni muhimu kwamba maandiko yawe mwongozo wetu badala ya kutumia akili ama falsafa ili kuelewa jambo hilo. Maandiko yanaashiria wakati ambapo Yesu atarudi. Wakati huo kila mtu atafufuka, kutakuwa na hukumu ya watu wote, na pia watu watapewa adhabu na thawabu za milele, nayo dunia itaangamizwa.

### Yesu atarudi


Yesu aliwaambia wanafunzi wake “Nitakuja tena” (Yohana 14:3, 28). Malaika wa Mungu alisisitiza ukweli huo wakati Yesu alipopaa kwenda mbinguni baada ya kufufuka (Matendo 1:11). Yesu atarudi kama mwizi usiku (1 Wathesalonike 5:2) wakati hakuna mtu anamtarajia. Kuna watu wengi wanaoitwa manabii ambao wamejaribu kutoa tarehe ya wakati Bwana atakaporudi, “Walakini habari ya siku ile na saa ile hakuna aijuaye, hata malaika walio mbinguni, wala Mwana, ila Baba” (Marko 13:32). Hii ndiyo sababu kila mtu anahitaji kwa mwangalifu na kuwa tayari kwa kurudi kwa Bwana, “…kwa kuwa saa msiyodhani ndipo ajapo Mwana wa Adamu” (Luke 12:40).

### Wakati utafika mwisho

Itakuwa siku yenye utukufu mwingi lakini pia majonzi mengi wakati Yesu atakaporudi na kuumaliza ulimwengu. Watakatifu watafurahi na wasiokuwa watakatifu walie kwamba mawe na milima iwaangukie. Yesu atapenya kwenye mawingu na “kila jicho litamwona” (Ufunuo 1:7). “Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu…” (1 Wathesalonike 4:16). Atakuja “katika utukufu wa Baba yake pamoja na malaika zake” (Mathayo 16:27).

### Wafu watafufuka

Wakati Yesu atakaporudi mawinguni watu wote watafufuka kutoka kwa wafu: “Kwa dakika moja, kufumba na kufumbua, wakati wa parapanda ya mwisho; maana parapanda italia, na wafu watafufuliwa, wasiwe na uharibifu, nasi tutabadilika” (1 Wakorintho 15:52). Ingawa kuna watu wengi wanaofundisha kwamba ni watakatifu tu watafufuliwa maandiko hufunza kwamba “kutakuwa na ufufuo wa wafu, wenye haki na wasio haki pia” (Matendo 24:15). “Msistaajabie maneno hayo; kwa maana saa yaja, ambayo watu wote waliomo makaburini wataisikia sauti yake. Nao watatoka; wale waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima, na wale waliotenda mabaya kwa ufufuo wa hukumu” (Yohana 5:28-29).



## HUKUMU

*“Kwa kuwa imeandikwa,*
*Kama niishivyo, anena Bwana, kila goti litapigwa mbele zangu;*
*Na kila ulimi utamkiri Mungu.”*

*Warumi 14:11*

### Dunia itaangamizwa

Neno la Mungu linafunza kwa njia dhahiri kabisa kwamba ulimwengu huu utaangamizwa (Mathayo 24:35; Waebrania 1:10-11). Petro wa Pili 3:7 nayo inasema, “Lakini mbingu za sasa na nchi zimewekwa akiba kwa moto, kwa neno lilo hilo, zikilindwa hata siku ya hukumu, na ya kuangamia kwao wanadamu wasiomcha Mungu.” Wakati Yesu atakaporudi ili kumletea mwanadamu hukumu mbingu za juu na dunia itapita na kuchomwa. Ulimwengu utatoweka na viumbe vitauguzwa kwa moto mkubwa (2 Petro 3:10-12).

*(Inaendelea kutoka ukurasa 6)*

*(Endelea kutoka ukurasa 5)*

### Kila mtu atasimama mbele zake Mungu

Katika siku hiyo ya mwitho, ambayo ni siku ya Bwana, Kristo atauhukumu ulimwengu. Yeye ndiye "atakayewahukumu walio hai na waliokufa; kwa kufunuliwa kwake" (2 Timotheo 4:1). Watu wote wa kila kizazi, wa kila kabila, wa kila lugha, wa kila taifa, watasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo. Kila mtu wa kila imani na dini atasujudu na kukiri kwamba Yesu ni Bwana (Warumi 14:10-12). Hukumu hii itakuwa ya ajabu na kuogofya huku kila mtu akiwajibika mbele zake Mungu. Siri zote zitawekwa wazi na hakuna kitakachokuwa kimejificha (Mhubiri 12:14).




### Kutakuwa na hukumu moja ya mwisho

Onyesho moja la hukumu ambalo lina uzito makubwa linaonekana katika Mathayo 25:31-46 na pia katika Ufunuo 20:11-15. "Na mataifa yote watakusanyika mbele zake; naye atawabagua kama vile mchungaji abaguavyo kondoo na mbuzi" (Mathayo 25:32). Watu wote wakisimama mbele zake Mungu kitabu cha uhai kitafunguliwa (Ufunuo 20:12) na kila mtu atahukumiwa na neno la Mungu (Yohana 12:48) na atapokea thawabu ama adhabu yake "kadiri alivyotenda, kwamba ni mema au mabaya" (2 Wakorintho 5:10).

Thawabu na adhabu za milele zitatolewa katika hukumu hiyo ya mwisho. Hatma yetu ya milele itategemea uchaguzi ambao tunafanya katika maisha haya. "Tazama, naja upesi, na ujira wangu u pamoja nami, kumlipa kila mtu kama kazi yake ilivyo" (Ufunuo 22:12). Mungu atatoa hukumu na ni yeye "atakayemlipa kila mtu kwa kadiri ya matendo yake" (Warumi 2:6). Kulingana na kiwango cha jinsi mtu anamwelewa Mungu na ukweli, ndivyo atakavyotakiwa kuwajibika na atapata adhabu kwa kiwango hicho ikiwa yeye ataukataa ukweli huo: "Na mtumwa yule aliyejua mapenzi ya bwana wake, asijiweke tayari, wala kuyatenda mapenzi yake, atapigwa sana. Na yule asiyejua, naye amefanya yastahiliyo mapigo, atapigwa kidogo. Na kila aliyepewa vingi, kwake huyo vitatakwa vingi; naye waliyemwekea amana vitu vingi, kwake huyo watataka na zaidi." (Luka 12:47-48). (Tazama pia: 2 Petro 2:21; Waebrania 10:26-29; na Mathayo 11:20-24).

### Wale ambao si watakatifu wataenda Jehanamu kudumu huko milele

Mungu amewahifadhi "wasio haki katika hali ya adhabu hata siku ya hukumu" (2 Petro 2:9). Adhabu ya waovu itakuwa huko Jehanamu (Zaburi 9:17). Jehanamu ni mahali pa mielele, pa maangamizi ya milele (2 Wathesalonike 1:9). Katika Ufunuo 21:8 Jehanamu imepewa mfano wa "ziwa liwakalo moto na kiberiti." Hapo kwenye hukumu Yesu atamwambia mwenye dhambi: "Ondokeni kwangu, mliolaaniwa, mwende katika moto wa milele, aliowekewa tayari Ibilisi na malaika zake" (Mathayo 25:41). Patakuwa mahali pa "kilio na kusaga meno" (Mathayo 24:51). Kwa kuwa hakutakuwa na kitu kizuri mahali hapo hakuna mtu aliye huko ambaye ataweza kuhepa uchungu, maumivu, kumbukumbu, na giza hilo la milele.

### Walio-okoka wataingia mbinguni na kudumu huko milele

Wakati watu wasio watakatifu wataingia adhabu ya milele, watakatifu watarithi uzima wa milele (Mathayo 25:45-46). Kuna "Urithi usioharibika, usio na uchafu, usionyauka, uliotunzwa mbinguni kwa ajili yenu" (1 Petro 1:4). Mungu ameandaa mji wa mbinguni (Waebrania 11:6) ambao maneno ya maisha haya ya kisasa hayawezi kuuelezea (2 Wakorintho 12:4). Ni mji wa angani wa hali ya juu sana, na urembo wake ni mkubwa mno na ambao ndani mwake kuna mambo yote mema na ya haki ambayo ni thawabu ya watakatifu. (Tazama pia Ufunuo 21 and 22).

—mws

# SWALI na JIBU

**Swali: Je, kutakuwa na utawala wa miaka elfu moja?**

**Jibu:** Hili ni swali ambalo linafaa kwa sababu kuna hali kubwa ya kuchanganyikiwa na hata mafundisho ya uwongo kuhusiana na kuja kwa pili kwa Kristo. Jibu la swali nilo ni "hapana." HAKUTAKUWA NA UTAWALA WA MIAKA ELFU MOJA.

Ingawa madhehebu mbali mbali yana imani tofauti kuhusiana na swala hili, dhana ya utawala wa miaka elfu moja huhusisha mafundisho kwamba Kristo atarudi duniani na kuanzisha "Ufalme wa Miaka Elfu Moja." Wenye dhana hii wanaamini kwamba Yesu, huku akiwa na makao makuu huko Yerusalemu, atatawala juu ya mataifa ya dunia kwa miaka elfu moja kabla ya hukumu ya mwisho kufanyika. Lakini jambo hili ni kinyume na mafundisho dhahiri ya maandiko kuhusu kurudi kwa Kristo na sifa za Ufalme wa Mungu.

HAKUNA HAJA YA UTAWALA WA MIAKA ELFU MOJA kwa maana Kristo tayari ashaanzisha utawala wake. Yesu alisema katika Yohana 18:36, "Ufalme wangu sio wa ulimwengu huu. Kama ufalme wangu ungekuwa wa ulimwengu huu, watumishi wangu wangenipigania . . ." Wakati Mafarisayo walitaka kujua ufalme wa Mungu ungekuja lini Yesu alijibu kwa kuwaambia, "Na alipoulizwa na Mafarisayo, Ufalme wa Mungu utakuja lini? Aliwajibu akawaambia, ufalme wa Mungu hauji kwa kuuchunguza; wala hawatasema, Tazama, upo huku, au, kule, kwa maana, tazama, ufalme wa Mungu umo ndani yenu" (Luka 17:20-22). Ufalme wa Mungu ni ufalme wa kiroho. "Maana ufalme wa Mungu si kula wala kunywa, bali ni haki na amani na furaha katika Roho Mtakatifu" (Warumi 14:17). Ufalme wa kidunia wa Yesu Kristo ulianzishwa katika mioyo ya waumini wakati alipokuja mara ya kwanza. Watu wa Mungu wanatawala sasa (Warumi 5:17). Kazi ya duniani ya Yesu ilimalizika alipokuja mara ya kwanza, "Mimi nimekutukuza duniani, hali nimeimaliza kazi ile uliyonipa niifanye" (Yohana 17:4). Wale ambao wanaamini utawala wa miaka elfu moja huwa na maoni yenye upotovu kwamba Kristo atakaa kwenye kiti cha enzi cha Daudi katika siku sijazo. Kusema kweli kiti cha utawala wa Daudi kiliangamia miaka mingi iliyopita. Kiti cha utawala cha Daudi kinawakilisha nguvu za utawala wa kifalme. Yesu alizaliwa "Mfalme wa Wayahudi" (Mathayo 2:2). Wakati Yesu aliingia Yerusalemu kusanyiko walipaza sauti wakisema, "Hosana; ndiye mbarikiwa ajaye kwa jina la Bwana; umebarikiwa na ufalme ujao, wa baba yetu Daudi. Hosana juu mbinguni" (Marko 11:9-10).

***"Kulingana na maandiko hamna haja ya utawala wa miaka elfu moja,***



***hamna pia wakati wa utawala huo, na hakuna mahali pa kuwa na utawala huo."***

HAKUTAKUWA NA WAKATI WA UTAWALA WA MIAKA ELFU MOJA wakati Kristo atakaporudi. Wakati huo kutakuwa na ufufuo moja wa wafu (Yohana 5:28-29) katika siku ya mwisho (tazama Yohana 6:39-40, 44, 54). Hakutakuwa na ufufuo tofauti ya watakatifu na waovu. Kristo atawahukumu watu wote pamoja (Mathayo 25:31-34, 41, 46) ambapo watapata thawabu za milele. Jambo hili litatendeka hapo 'siku ya mwisho.'

HAKUTAKUWA NA MAHALI PA UTAWALA WA MIAKA ELFU baada ya Kristo kuonekana. Tazama andiko la 2 Petro 3:7,10: "Lakini mbingu za sasa na nchi zimewekwa akiba kwa moto, kwa neno lilo hilo, zikilindwa hata siku ya hukumu, na ya kuangamia kwao wanadamu wasiomcha Mungu . . . Lakini siku ya Bwana itakuja kama mwivi; katika siku hiyo mbingu zitatoweka kwa mshindo mkuu, na viumbe vya asili vitaunguzwa, na kufumuliwa, na nchi na kazi zilizomo ndani yake zitateketea." Maandiko yanasema kwa uwazi kabisa kwamba Yesu atakaporudi ulimwengu huu utaangamizwa kabisa kwa moto. Jambo hilo litatendeka katika siku hiyo ya hukumu wakati Bwana atakaporudi kama mwizi wa usiku.


Kulingana na maandiko hamna haja ya utawala wa miaka elfu moja, hamna pia wakati wa utawala huo, na hakuna mahali pa kuwa na utawala huo. Mafundisho kuhusu utawala huo ni udanganyifu kutoka kwa adui yetu. Wengi wanatafuta na kutumaini kupata nafasi nyingine katika siku sijazo. Lakini hakuna nafasi ya pili kwa maana hii ndiyo siku ya wokovu. Huu ndio wakati wa mtu kuingia katika ufalme wa Mungu na kujiandaa kwa sababu ya siku zake za milele.

—mws

## JE, WAJUA?

**Maandiko:** Matendo 2:27 Kwa maana hutaiacha roho yangu katika kuzimu (jehanamu); wala hutamtoa Mtakatifu wako aone uharibifu. (Andiko linalofanana na hilo ni: Zaburi 16:10).

*'Jehanamu'* kwenye andiko hili limetafsiriwa kutokana na neno la Kiyunani *'Kaburini'* na pia kutokana na neno la Kiebrania la '*Kuzimu.'* Maneno haya yanamaanisha: *kaburi, hali ya walio wafu, au mahali pa nafsi zilizoondoka.*



Wakati Yesu aliposulubishwa msalabani hakwenda jehanamu ya shetani. Nafsi yake ilipaa hadi paradiso—mahali pa furaha na starehe.

Yesu alimwambia mwizi pale msalabani, "Leo hivi utakuwa pamoja nami peponi" (Luka 23:43).

Neno Linalofaa kwa Msimu Huu

# Ingia Katika Furaha ya Bwana Wako

*Bwana wake akamwambia, Vema, mtumwa mwema na mwaminifu; ulikuwa mwaminifu kwa machache, nitakuweka juu ya mengi; ingia katika furaha ya bwana wako.* —Mathayo 25:23

Haya ni maneno ya ajabu kwa mtumishi aliye mwaminifu kwa Mungu kuyasikia huku akisimama mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu: "ingia katika furaha ya bwana wako." Mashindano yote, uchungu wote, hali za kufisha mtu moyo, masikitiko, majaribu ya maisha haya, hayo yote yanaonekana kama si chochote tutakapoingia mahali pale pa urembo mkuu panapoitwa "Mbinguni," ambapo Mungu amewaandalia watu wake.



Matarajio ya Mbinguni huendelea kung'aa zaidi kwa mtakatifu wa Mungu. Kunakuja siku ambayo hakutakuwa na kifo, majonzi moyomi, machozi, na magonjwa, na hata hali za kutojiweza, majaribu, na hata shida. Kunakuja siku ambayo kutakuwa na utukufu, urembo, na furaha mbele ya uwepo wake Mfalme wa Wafalme na Bwana wa Mabwana.

Hakutakuwa na haja ya jua kwa sababu Mwanakondoo atakuwa mwanga wao. Utukufu wake utazidi wote ule ambao mawazo ya mwanadamu yanaweza kuwazia, na wote ambao unaweza kustahimiliwa na mwanadamu. Bas siku hiyo watumishi wa Bwana watakuwa na mwili uliotukuzwa, katika siku hiyo kuu ya ufufuo, ili waweze kupata ujuzi na utukufu kamili na wa milele wa huko Mbinguni.

Basi wewe mtumishi wa Bwana ninakuomba uwe mwaminifu na imara. Mbingu itakuwa zaidi ya masaibu ote unayopitia.

—mws

**Anwani**

The Gospel Truth
P. O. Box 2042
Nixa, MO 65714
USA
Email:
editor@thegospeltruth.org

Utakatifu kwa Bwana